

# Zama ni mkubwa!

## Zama is great!

- ✎ Michael Oguttu
- ⌚ Vusi Malindi
- 💬 Matteo E. Mwita
- 💬 Kiswahili / English
- 📊 Level 2

(imageless edition)





Mdogo wangu anachelewa  
kuamka. Mimi naamka mapema  
kwa sababu mimi ni mkubwa!

...

My little brother sleeps very late. I  
wake early, because I am great!



Mimi ndiye ninayeruhusu jua  
kuingia ndani.

...

I am the one who lets in the sun.



“Wewe ni nyota wangu wa  
asubuhi,” anasema mama.

...

“You’re my morning star,” says  
Ma.



Naoga mwenyewe, sihitaji msaada.

...

I wash myself, I don't need any help.



Naweza kustahimili maji ya baridi  
na sabuni ya bluu inayonuka.

...

I can cope with cold water and blue  
smelly soap.



Mama ananikumbusha, "Usisahau  
kupiga mswaki." Namjibu,  
"Kamwe, sio mimi!"

...

Ma reminds, "Don't forget teeth." I  
reply, "Never, not me!"



Baada ya kuoga, nawasalimu babu na shangazi, na kuwatachia siku njema.

...

After washing, I greet Grandpa and Auntie, and wish them a good day.



Najivisha nguo mwenyewe. "Mimi  
ni mkubwa sasa mama,"  
ninamwambia.

...

Then I dress myself, "I'm big now  
Ma," I say.



Ninaweza kufunga vishikizo na  
kurekebisha viatu vyangu.

...

I can close my buttons and buckle  
my shoes.



Na ninahakikisha mdogo wangu  
anapata taarifa zote za shule.

...

And I make sure little brother  
knows all the school news.



Darasani najitahidi sana katika kila  
kitu.

...

In class I do my best in every way.



Ninafanya hivi vitu vyote vizuri kila siku. Ila kitu ninachokipenda sana ni kucheza na kucheza.

...

I do all these good things every day. But the thing I like most, is to play and play!



# Storybooks Canada

[storybookscanada.ca](http://storybookscanada.ca)

Zama ni mkubwa!

Zama is great!

Written by: Michael Oguttu

Illustrated by: Vusi Malindi

Translated by: (sw) Matteo E. Mwita

This story originates from the African Storybook ([africanstorybook.org](http://africanstorybook.org)) and is brought to you by [Storybooks Canada](#) in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons  
[Attribution 3.0 International License](#).